

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA  
Simu Na: +255 26 2321607  
Nukushi: +255 26 2322116  
Barua pepe:[ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Mtaa wa TAMISEMI,  
S.L.P. 1923,  
41185 DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA**

**UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA  
KWANZA MWAKA 2023 KWA WANAFUNZI WALIOFANYA MTIHANI WA MARUDIO  
TAREHE 21 – 22 DESEMBA 2023**

Baraza la Mitihani la Tanzania lilitoa taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Marudio kwa wanafunzi wa Darasa la Saba mwaka 2022 ambapo jumla ya wanafunzi **2,194** wakiwemo wavulana **1,117** na wasichana **1,077** walitakiwa kufanya mtihani huo kuanzia tarehe 21 – 22 Disemba 2022 kwa sababu matokeo yao yalifutwa kwa mujibu wa kifungu **30(2)(b)** cha Kanuni za Mitihani 2016 kikisomwa pamoja na kifungu cha **5(2)(i)** na **(j)** cha sheria cha Baraza la Mitihani Sura ya **107**. Jumla ya wanafunzi **2,180** wakiwemo wavulana 1,112 na wasichana 1,068 sawa na asilimia **99.36** walifanya mtihani wa marudio.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea matokeo ya mtihani huo ambapo jumla ya wanafunzi **2,096** wakiwemo wavulana ni **1,073** na wasichana ni **1,023** sawa na asilimia **96.15** ya watahiniwa waliofanya mtihani wamepata sifa ya kuchaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza katika Shule za Sekondari za Serikali. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Kamati za Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza katika mikoa husika imekamilisha zoezi la kuwapangia Shule wanafunzi wote **2,096** katika Shule mbalimbali za Sekondari. Maandalizi ya kuwapokea wanafunzi hao yamekamilika na wanataarifiwa kuripoti katika Shule walizopangiwa siku ya Jumatatu tarehe 16 Januari 2023 ili kuanza masomo. Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz).

Mwanafunzi, Mzazi/Mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelekezo au ufanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri au apige simu kwenye Kituo cha Huduma kwa Wateja, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa namba za simu **026 2160210** au **0735 160210**.

Imetolewa na

**KATIBU MKUU**  
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**  
13 Januari 2023